**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Shule ya Sekondari Kagemu,
S. L. P. 1232,
**BUKOBA**.
29/03/2022

**Namba za simu:**
Mkuu wa shule: 0752 609946/0675238934
Makamu Mkuu wa shule: 0765520961/0679165178
Matron:0768 318 158/0757 752598

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi… … … … … … … … … … … … … … … … … ..
… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ..
S. L. P… … … … … … … … … … … … … … … … … …

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAGEMU HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA MKOA KAGERA 2021**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022/2023 tahasusi ya … … … … … … … … … . Shule ya Sekondari Kagemu ipo umbali wa kilometa 5 Magharibi mwa mji wa Bukoba. Usafiri wa taksii kutoka Bukoba mjini hadi shuleni ni kuanzia Tshs 5,000 ☐ 10,000 bajaji si chini ya 4,000/= na usafiri wa pikipiki si zaidi ya shs 1,500/=.

Muhula wa masomo unaanza tarehe … … … … … … … … … … … ..Hivyo mwanafunzi anatakiwa shuleni tarehe… … … … … … … … … mwisho wa kuripoti ni tarehe… … … … … … … … … … … … ..

1. **Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1: Sare ya shule (Uniform)**

i) Shati nyeupe 2 zenye mikono mirefu na zisizo na urembo wowote
ii) Soksi nyeupe jozi 2
iii) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi vyenye kufunika miguu na visivyo na urembo wowote jozi 2.
iv) Nguo za michezo ambazo ni ☐track suit☐ ya kijivu kitambaa kizito na raba jozi moja.

v) Sweta rangi ya kijani (dark green) yenye vifungo (vishikizo) vinne ( 4 ).
vi) Tai iwe rangi ya skirt damu ya mzee isiyo na michirizi yoyote.
vii) Sketi Damu ya mzee (2) kitambaa kizito (Fsteem) yenye mshono wa malinda box (8 mbele na 8 nyuma), kwa waislam washone sketi ndefu na hijabu inayofunika kifua (Angalia picha iliyoambatanishwa)
viii) Nguo za nje ya darasa (shamba dress) Gauni 2 draft ya blue/nyeupe ( kunguru) kitambaa cha tetron nzito. Mshono wa soro na shingo ya duara, rejea mchoro.
ix) T-shirt☐ rangi ya bluu bahari ( light blue) yenye shingo ya duara kitambaa kizito.

2. **Ada na michango ya shule**

a) Ada ya shule shs 35,000/= kwa muhula (70,000/=) kwa mwaka

b) Michango mingine

- Taaluma shs 10,000/= kwa muhula (20,000/= kwa mwaka)
- Kitambulisho na picha shs 6,000/=
- Tahadhari shs 5,000/= kwa muhula (haitarejeshwa)
- Nembo ya shule shs 2,000/=
- Fedha ya kuwalipia wapishi, walinzi na vibarua wengine shs 15,000/= kwa muhula (30,000/= kwa mwaka)
- Ukarabati wa samani shs 15,000/=
- Huduma ya kwanza shs 10,000/=
- Mitihani ya kujipima (Mock) shs 20,000/=

Jumla ya ada na michango kwa mwaka ni shs 178,000/= (Laki moja sabini na nane elfu tu)

NB. Fedha hizo zote zilipwe kwenye akaunti ya shule:

Namba ya akaunti **31801100125 Benki ya NMB**. Jina lal akaunti ni **KAGEMU SECONDARY SCHOOL.** Mwanafunzi awasilishe nakala ya malipo iliyoandikwa jina lake wakati wa kuripoti.

**c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**

i) Madaftari makubwa yasiyopungua 10 (counter books) Q3
ii) Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)
iii) Rula, kalamu za wino na pencil za kutosha muhula
iv) Dictionary/kamusi (kwa wanafunzi wa sanaa)
v) Karatasi (Photocopy papers-A4) Ream 1 kwa muhula (2 kwa mwaka)
vi) Scientific calculator (wanafunzi wa sayansi)
vii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
viii) Mwavuli wa mvua mmoja (1)
ix) Mto mmoja (1) na foronya mbili (2) za rangi ya pinki
x) Mashuka manne (4) ya pinki yasiyo na maua na blanketi moja (1)
xi) Godoro moja (1) la futi 3 na chandarua kimoja (1) cha mraba
xii) Jozi mbili (1) ya kanga/vitenge

xiii) Sahani 1, bakuli 1, kikombe 1, kijiko 1, vyombo vyote viwe vya bati/mfupa

xiv) Toilet papers (karatasi za chooni) kumi (10)

xv) Kifaa cha maji ya kunywa (kidumu kidogo lita 3 au 5)

xvi) Taulo (1)

xvii) Nguo za ndani (gagulo 2, chupi zisizopungua 6 na sidiria 3)

xviii) Vifaa maalum vya matumizi ya msichana (Always paketi 4)

xix) Sabuni,mswaki, dawa ya meno, mafuta ya kujipaka, dawa ya viatu

xx) Fyekeo 1, jembe 1, kotama au Rake, mifagio ya ndani 1 na brush ngumu (ndefu/fupi) ya kusugulia vyoo 1, na mopa 1.

xxi) Ndoo ya kuchotea maji yenye ujazo wa lita 20 na beseni moja la kuogea

xxii) Fedha kidogo za matumizi binafsi maana shule hutoa chakula.

xxiii) Night dress 1

**3. Viambatisho na fomu muhimu**

Binti yako atatakiwa kukamilisha na kuleta viambatisho au fomu kama ifuatavyo:

**a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form)**

Ni lazima binti yako apimwe katika Hospitali ya Serikali ya wilaya au mkoa na si zahanati na daktari anayehusika ili kukamilisha vipengele vya afya yake. Fomu hii ni lazima iwasilishwe shuleni mara anaporipoti.

b) **Cheti cha Uraia** ☐ Alete cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate) au cheti cha utambulisho wa uraia ambacho hupatikana kwa Mkuu wa Wilaya yako. Kumbuka hatutakubali utambulisho wa vijiji, Kata au Tarafa.

c) **Taarifa Binafsi** ☐ Fomu maalum imeambatanishwa, fomu hii ijazwe kwa uangalifu na kurudishwa hapa shuleni anapokuja kuripoti.

d) **Picha za utambulisho wa wazazi na walezi** ☐ weka picha za hivi karibuni kwenye chumba husika kama ilivyo kwenye taarifa binafsi kipengele B, C na D. Hatasikilizwa mzazi au mlezi kwa shauri lolote linalohusu mwanafunzi iwapo taarifa binafsi haitajazwa kwa ukamilifu na kuweka picha.

NB. Mwanafunzi alete hati ya matokeo (result slip) yake ya kidato cha nne akiwa ametoa copy.

**4. Mambo mengine muhimu ya kuzingatia**

Kuna likizo fupi mbili kwa mwaka, wakati huu shule huruhusu vijana wa karibu kwenda nyumbani na wengine kubaki shuleni. Kuondoka bila ruhusa ni utoro. Pia kuna likizo mbili ndefu, wakati huo kila mwanafunzi anaruhusiwa kwenda kwao. Shule huwaruhusu vijana wote ili wasafiri kwenda kwa wazazi/walezi wao na siyo kwingineko. Ni mategemeo ya shule kuwa wakati huu vijana watatumia muda wao vizuri kwa kuwasaidia wazazi kufanya shughuli mbalimbali za kuzalisha mali na kusoma, kuliko kuzurura ovyo.

Ni sheria ya shule kwamba baada ya likizo kila mzazi ahakikishe mtoto wake anawahi shuleni katika siku na tarehe zilivyopangwa na analeta mahitaji yote muhimu. Akichelewa aje na mzazi/mlezi au barua ya mzazi/mlezi ikieleza sababu ya kuchelewa la sivyo atachukuliwa hatua za kinidhamu.

**5. Mwisho:**

Hakikisha umekamilisha mahitaji yote na kujaza fomu zote kabla ya kumleta mtoto shuleni, cheti cha uraia, fomu ya taarifa binafsi na fomu ya Afya na sheria za shule zilizotiwa sahihi. Lazima virudishwe shuleni. Kwa niaba ya jumuiya nzima ya shule ya sekondari Kagemu napenda kumpa hongera binti yako kwa kufaulu mitihani na kuchaguliwa kujiunga na shule hii. Tunauhakika akifuata sheria za shule na akasoma kwa bidii na kwa malengo atafanikiwa.

**KARIBU SANA .**

Loyce M. Ngeleja

**MKUU WA SHULE**

**6.0: SHERIA ZA SHULE** ***KIAMBATISHO A***

**JINA LA MWANAFUNZI□□□□□□□□□□□□□□□KIDATO CHA□□MWAKA□□□□□□□□□.**

**a) Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule:**

i) Wizi

ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa au utoro

iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu au walezi na jamii kwa ujumla

v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule

vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule (mistari ya kwenda nyuma 3, 5 au 7)

vii) Ulevi wa kunywa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

viii) Kudharau Bendera ya Taifa

ix) Uvutaji bangi/sigara/ugoro

x) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja na kuolewa

xi) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu au laini ya simu ya mkononi katika mazingira ya shule

xii) Kupata ujauzito au kutoa mimba

xiii) Kutembelea majumba ya starehe, nyumba za waalimu au za kulala wageni

xiv) Kufanya jaribio lolote kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

xv) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi

xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

**b) Mwanafunzi awapo shuleni/hapaswi kufanya yafuatayo**

- Kufuga kucha ndefu
- Kupaka rangi kwenye kucha, mdomo,kope au nyusi
- Kutumia vipodozi
- Kukata au kusuka nywele kwa mitindo iliyo tofauti na maelekezo ya mwandamizi wa malezi na Utamaduni

- Kuvaa nguo fupi au zinazobana mwili
- Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- Kumiliki kifaa chochote kinachotumia umeme kama pasi, heater, redio n.k

**c) Mwanao awapo shuleni atatakiwa:**

- Kuhudhuria vipindi vyote bila kukosa
- Kuvaa sare ya shule/ya kazi wakati wote
- Kutii amri na sheria zote za shule
- Kujiheshimu, kuheshimu wenzake, viongozi, walimu na watu wote kwa ujumla
- Kutunza mali zake na mali za umma

**d) Heshima**

i) Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuamkia walimu, wafanyakazi wasio walimu pia mtu au mgeni yoyote anayemzidi umri anapopita na anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

ii) Mwanafunzi kama raia mwema, lazima aheshimu Bendera ya nchi yake na wimbo wa Taifa

iii) Matusi, lugha chafu na kupigana ni dalili ya kukosa heshima

**e) Utii**

i) Kila mwanafunzi hana budi atii na kufuata maelekezo na maagizo ya viranja, walimu na wafanyakazi wasio walimu na watu wote

ii) Mwanafunzi anapoitwa Mahali lazima aitike na kukimbia kuelekea kule aliko kiongozi anayemuita ikiwa ni mahali salama.

iii) Kiburi, majibu ya jeuri na matumizi ya lugha mbaya haviruhusiwi

iv) Ni wajibu kila mwanafunzi kufanya na kukamilisha kazi anayopangiwa iwe nje au ndani ya darasa

**f) Upendo**

Mwanafunzi ajipende yeye mwenyewe na awapende wenzake kama ndugu zake wa shuleni awapende walimu kama wazazi wake, aipende shule yake kama nyumbani kwake, aipende na kujivunia nchi yake ya Tanzania.

**g) Ruhusa**

Ruhusa maalum ya kutoka nje ya shule itatolewa mara moja kwa muhula (shopping day) kutegemea na uongozi utakavyoamua.

**h) Mambo ya msiba**

Mwanafunzi akifiwa akiwa shuleni ataruhusiwa kuomboleza shuleni tu. Taarifa zote za kilio zitapashwa zipitie kwenye ofisi ya Mkuu wa shule. Ruhusa ya kwenda nyumbani itatolewa na Mkuu wa shule baada ya kuzingatia taratibu muhimu.

**i) Mabadiliko ya anwani**

Unashauriwa kutoa taarifa kwa Mkuu wa shule iwapo anwani inayotumika kwa mawasiliano imebadilika.

**j) Ripoti**

Shule hatuna taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitabia isipokuwa taarifa za kitaaluma zitatumwa kila muhula. Tafadhali hakikisha unaipata na kutuma maoni yako shuleni.

**k) Utumaji wa fedha binafsi za binti yako**

Wazazi wanaowatumia watoto wao fedha za matumizi wafanye hivyo kwa kutumia Posta kwa njia ya ☐Money Fax☐ au kwa M-Pesa kwenye Namba 0752609946, 0768318158 ,0757 752598, taarifa za kuwataka wanafunzi kufuata fedha zilizotumwa kupitia kwa jamaa zao wanaokaa nje ya shule hazitakubaliwa.

JE UNAKUBALI? NDIYO ☐ HAPANA ☐

(Weka alama √ panapo husika)

Jina la Mwanafunzi.........................................Sahihi.....................Tarehe.................

Jina la Mzazi/Mlezi.........................................Sahihi.....................Tarehe.................

***KIAMBATISHO B***

ANUANI.............. … … … … … … … … …

… … … … … … … … … … … … … … … … … … … **..**

… … … … … … … … … … … … … … … … … … … …

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Kagemu,
S. L. P. 1232,
**BUKOBA.**

**TAARIFA BINAFSI**

A. Jina la Mwanafunzi… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …

Anwani ya nyumbani… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … **.**

… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … **..**

Kabila… … … … … … … … … … … … … … … … … … … Mwaka aliozaliwa… … … … … … … … … … … … … … … … …

Mtanzania/Si Mtanzania

Dini ya mwanafunzi… … … … … … … … … **.**Mtaa/Kijiji… … … … … … … … … Jina la mratibu elimu kata/Mtendaji… … … … … … … … … … … … … … **..**namba za simu… … … … … … … … … … … … … … … Wilaya… … … … … … … … … … … … … **..**Mkoa… … … … … … … … … … … … … … …

B. Jina la Baba… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … **..***(Hai/Marehemu)… … … … … … … … … …

(mwaka aliofariki)… … … … … … … … … … … … … **..**

Dini ya Baba… … … … … … … … … … … … … kazi ya Baba… … … … … … … … … … Simu Na… … … … … … … … … …

Jina la mama… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … *(Hai/Marehemu)… … … … … … … … …

Dini ya mama… … … … … … … … … … … … … kazi ya mama … … … … … … … … … … ..Sim Na… … … … … ..

mwaka aliofariki… … … … … … … … … …

C. Taja majina na anuani za walezi/Ndugu wengine wawili wasiokuwa wazazi wanaoruhusiwa kufika shuleni kuyasikiliza na kutoa maamuzi juu ya mashauri ya mtoto wako.

JINA… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … .ANUANI… … … … … … … … … … … ..SIMU NA… … … … … … .

JINA… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … .ANUANI… … … … … … … … … … … ..SIMU NA… … … … … … .

D. Taja majina ya watu watakaoruhusiwa kumtembelea mtoto wako akiwa hapa shuleni

1… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … Uhusiano… … … … … … … … umri… … … … … … .simu… … … … … … … ..

2… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … Uhusiano… … … … … … … … .umri… … … … … … ..simu … … … … … … … .

3… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … Uhusiano… … … … … … … … .umri… … … … … … ..simu … … … … … … …

**B. Picha za wazazi**

| | |
|---|---|
| | |

**C. Picha za walezi**

| | |
|---|---|
| | |

**D. Picha za ndugu wengine kama wapo (sio lazima kama wanne wanatosha)**

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |

***KIAMBATISHO C***

## MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING FORM FOR STUDENT MEDICAL EXAMINATION

Student☐s Name… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …..

Blood Examination: Haemoglobin… … … … … … … … … … … … … … … ..Blood Group… … … … … …

Stool Examination… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ….

Urinalysis… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … .

T.B.Test (If negative, was immunization given)

Eyes… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …

Chest… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ..

Any chronic complaints not noted above e.g

Asthma… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … .

Headache… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …

Inability to eat certain foods… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ..

Skin disease etc… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … .

Also anything that the school health staff should know about… … … … … … … … … … … ..

… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ..

Any treatment given or recommended… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … .

… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ..


**NOTES:** If any of the examination requested above cannot be carried out, it is useful if it is noted that have not been done rather than writing **NAD** down. In case of Bilharzia it is recommended that students attend the Bilharzia clinic before they come to school.

Signature of Examiner… … … … … … … … … … … .

Designation… … … … … … … … … … … … … … … … ..

Date… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … .

**MICHORO NA PICHA**







Urefu wa sketi kutoka kwenye goti uwe cm 15 kwenda chini

Upana wa pindo la sketi uwe cm 6



